YALIYOMO

DIBAJI 3

1.1 Malengo ya Mwongozo 4

1.2 Malengo mahsusi 5

2.0 MAJUKUMU YA WIZARA NA SEKRETARIETI ZA MIKOA.... 5

2.1 Majukumu ya Wizara..... 5

2.2 Majukumu ya Mamlaka za Sekretarieti za Mikoa..... 5

3.0 MCHANGANUO WA MAJUKUMU YA MAAFISA USTAWI WA JAMII KATIKA NGAZI ZA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA 7

3.1 HUDUMA ZA USTAWI WA FAMILIA NA WATOTO; MALEZI, MAKUZI NA MAENDELEO YA AWALI YA WATOTO WADOGO NA WACHANGA..... 7

3.1.1 Huduma kwa Familia..... 7

3.1.2 Huduma za ustawi kwa Watoto..... 9

3.2 HUDUMA ZA MAREKEBISHO YA TABIA NA HAKI ZA MTOTO KISHERIA 15

3.2.1 Kusimamia Haki za Mtoto Kisheria..... 15

3.2.2 Kusimamia Huduma za Marekebisho ya Mtoto 16

3.2.3 Kusimamia huduma kwa watoto watukutu 17

3.2.5 Kusimamia Huduma kwa watoto wanaoishi na kufanya kazi Mitaani 17

3.3 HUDUMA KWA WAZEE NA WATU WENYE ULEMAVU..... 18

4.0 MAJUKUMU MENGINE MTAMBUKA 20

5.0 MAADILI YA AFISA USTAWI WA JAMII..... 20

6.0 HATUA MUHIMU ZA KUFUATA WAKATI WA UTENDAJI KAZI 22

7.0 HITIMISHO..... 22

KIAMBATISHO; Mfumo wa Utoaji Huduma za Ustawi wa Jamii katika Halmashauri..... Error! Bookmark not defined.

DIBAJI

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii) imepewa jukumu la kuratibu utoaji wa huduma za ustawi wa jamii hapa nchini. Katika kuwezesha utekelezaji wa jukumu hili Wizara imeandaa Mwongozo kwa Maafisa Ustawi wa Jamii katika Sekretariati za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Vituo vya kutolea huduma za ustawi wa jamii.

Katika utekelezaji wa Sera ya Ugatuaji wa Madaraka kutoka Serikali Kuu kwenda Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mikoa, Halmashauri zimekuwa zikiajiri Maafisa Ustawi Ustawi wa Jamii kwa ajili ya kuwezesha huduma za ustawi wa jamii kuwafikia wananchi. Hata hivyo pamoja na uwepo wa Sera, Sheria na Miongozo kumekuwepo na changamoto ya uelewa wa majukumu na mipaka ya utoaji wa huduma miongoni mwa wataalamu wa ustawi wa jamii. Hali hii imekuwa ikisababisha utoaji duni wa huduma na kukwamisha upatikanaji wa haki kwa makundi maalum.

Mwongozo huu umebainisha na kuainisha Sera, Sheria, Kanuni, Miongozo na Mikakati ya Kitaifa na Kimataifa inayoongoza huduma za ustawi wa Jamii hapa nchini. Aidha Mwongozo umeainisha majukumu ya Maafisa Ustawi wa Jamii kuanzia ngazi ya Taifa, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Vituo vya kutolea huduma za ustawi wa Jamii. Pamoja na kuainisha majukumu hayo, Mwongozo pia umebainisha maadili na hatua zinazotakiwa kufuatwa wakati wa kutoa wa huduma kwa walengwa.

Mwongozo huu ni chombo muhimu kwa watoa huduma za Ustawi wa jamii hapa nchini. Natoa wito kwa walengwa wa Mwongozo huu kutumia maelekezo yaliyo kwenye Mwongozo huu kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za ustawi wa jamii kwa makundi maalum.

Ni Matarajio ya Wizara kuwa Mwongozo huu utawawezesha Maafisa Ustawi wa Jamii katika ngazi zote kutekeleza majukumu yao kwa weledi na ufanisi.

.....

DKT. J.K. JINGU

KATIBU MKUU

(Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii)

1.0 UTANGULIZI

Huduma za Ustawi wa Jamii ni huduma zinazolenga kusaidia na kuwezesha makundi maalum kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo na kijamii. Makundi yanayolengwa na huduma hizi ni pamoja na Watoto Yatima na Walio katika Mazingira Hatarishi, Watoto Walio katika Mkinzano na Sheria, Watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani, Watu Wenye Ulemavu na Wazee. Makundi mengine ni yale ambayo yanakosa au yapo katika hatari ya kukosa fursa ya kushiriki kikamlifu katika shughuli za maendeleo mfano familia zenye migogoro ya ndoa, wakimbizi, watoto wanaokosa malezi bora, nk.

Huduma hizi zimekuwa zikitolewa kwa kuzingatia Sera, Sheria na Miongozo mbali mbali ambayo hutolewa na Serikali ili kuwezesha utoaji wa huduma bora za ustawi wa jamii zinazolenga kuboresha maisha ya watu walio katika makundi maalum. Katika kuwezesha utoaji wa huduma hizo kwa ubora na weledi, Mwongozo huu umeainisha majukumu mahsusi kwa Maafisa Ustawi wa Jamii na nyenzo zinazotumika katika kutoa huduma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na vituo vya kutolea huduma za ustawi wa jamii Nchini.

Kwa kuwa huduma za ustawi wa Jamii ni mtambuka, mbali na Sheria mbali mbali ambazo hutumika kama Mwongozo katika utoaji huduma, kuna Sera nyingine zinazozinazingatiwa ambazo ni pamoja na Sera ya Maendeleo ya Jinsia, Sera ya Elimu, Sera ya Hifadhi ya Jamii na Sera ya Afya. Vilevile utoaji wa huduma hizi unazingatia Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2015-2020), Sera mahususi za Wizara za Kisekta, Muundo wa Kada za Ustawi wa Jamii wa Mwaka 2009 pamoja na Mikakati ya Kitaifa na Mikataba ya Kimataifa ambayo imeridhiwa na kusainiwa na nchi inayohusu Haki za Watoto, Wazee na Watu wenye ulemavu.

1.1 Malengo ya Mwongozo

Lengo kuu la mwongozo huu ni kuimarisha utoaji wa huduma za ustawi wa jamii kwa kuwawezesha Maafisa Ustawi wa Jamii kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi, na kwa kuzingatia Sera, Sheria, na Miongozo ya Serikali. Mwongozo huu umezingatia aina ya

kazi zinazofanywa na Maafisa Ustawi wa Jamii, na utaratibu wa kutoa huduma.

1.2 Malengo mahsusi

(i) Kuwezesha Maafisa Ustawi wa Jamii katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na vituo vya kutolea huduma za ustawi wa jamii kutekeleza makujumu kwa ufanisi,

(ii) Kuongeza uwazi, uwajibikaji na ufanisi katika kutoa wa huduma za ustawi wa jamii kwa Nchini.

2.0 MAJUKUMU YA WIZARA NA SEKRETARIETI ZA MIKOA

2.1 Majukumu ya Wizara

Katika kuimarisha utoaji wa huduma za ustawi wa jamii nchini Wizara ina jukumu la kusimamia viwango vya ubora wa huduma hizo kwa kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo. Katika kuhakikisha utekelezaji wenye ufanisi Wizara inafanya yafuatayo;

(i) Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria na Miongozo ya utoaji huduma za ustawi wa jamii,

(ii) Kufanya tathmini, ufuatiliaji na uratibu wa huduma za ustawi wa jamii,

(iii) Kujenga uwezo wa kitaaluma kwa Maafisa Ustawi wa Jamii,

(iv) Kufanya tafiti zinazohusu huduma za ustawi wa jamii,

(v) Kuwajengea uwezo watumishi wa Ustawi wa Jamii na wadau katika kutoa wa huduma bora za ustawi wa jamii,

(vi) Kuanzisha na kuendeleza program za, kutetea na kulinda haki za makundi maalum,

(vii) Kujenga mahusuiano na wadau ili kuboresha huduma za ustawi wa jamii.

2.2 Majukumu ya Mamlaka za Sekretarieti za Mikoa

Sekretarieti za mikoa ndio wasimamizi wa huduma zote zinazotolewa katika ngazi za halmashauri, kata na vijiji/mitaa. Ni jukumu la msingi la mikoa kuhakikisha Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo inatekelezwa ipasavyo ili kuwawezesha wananchi kufikia huduma bora na zenye tija. Maafisa Ustawi

wa Jamii katika Sekretarieti za mikoa wana majukumu yafuatayo;

(i) Kuwa mjumbe na kushiriki katika kamati ya Mkoa ya Menejimenti ya Afya, kamati ya usimamizi wa huduma za afya (RHMT) na kamati nyingine zinazohusika na ustawi wa jamii,

(ii) Kushiriki na kupanga mipango ya kamati ya usimamizi wa huduma za afya (RHMT) na kutekeleza mipango ya mwaka,

(iii) Kuwezesha na kuzishauri halmashauri katika kutafsiri Sera, Sheria, na Miongozo inayohusiana na ustawi wa jamii kama ilivyoandaliwa na Wizara,

(iv) Kushirikiana na halmashauri kuweka mifumo ya kusaidia makundi yanayoishi kwenye mazingira hatarishi ili kupata huduma za msingi za kijamii,

(v) Kuziwezesha halmashauri kuhakikisha kuwa makundi yanayoishi kwenye mazingira hatarishi yanapata taarifa za mara kwa mara juu ya haki na ustawi wao,

(vi) Kushirikiana na halmashauri kuweka mifumo ya kuzuia na kupambana na majanga ya kijamii ambayo itasaidia upatikanaji wa huduma za kijamii,

(vii) Kuziwezesha halmashauri kuweka mipango itakayosaidia upatikanaji wa huduma za msingi kwa watu masikini, makundi yaliyotengwa pamoja na makundi ya watu wanaoishi kwenye mazingira hatarishi,

(viii) Kumshauri Katibu Tawala wa Mkoa kuhusu utoaji wa huduma bora za ustawi wa jamii kwa kuzingatia Sera, Sheria na Miongozo,

(ix) Kubuni na kupendekeza mipango mbalimbali ya utoaji wa huduma za ustawi wa jamii ndani ya mkoa,

(x) Kuandaa mipango na bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa huduma za ustawi wa jamii ndani ya mkoa.

3.0 MCHANGANUO WA MAJUKUMU YA MAAFISA USTAWI WA JAMII KATIKA NGAZI ZA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA

Maafisa Ustawi wa Jamii katika Mamlaka za Serikali za Mitaa wana mamlaka ya kusimamia na kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo mbali mbali katika maeneo makuu ya huduma kama ifuatavyo;

(i) Huduma kwa Familia, Watoto na malezi ya awali ya mtoto,
(ii) Huduma kwa Wazee na Watu wenye Ulemavu,
(iii) Huduma za Marekebisho ya Tabia na Haki za watoto kisheria.

3.1 HUDUMA ZA USTAWI WA FAMILIA NA WATOTO; MALEZI, MAKUZI NA MAENDELEO YA AWALI YA WATOTO WADOGO NA WACHANGA

Maafisa ustawi wa jamii wanayo dhamana ya kutoa Huduma za ustawi kwa familia na watoto; Malezi, Makuzi Na Maendeleo Ya Awali Ya Watoto Wadogo kwa kuzingatia Sera, sheria, Kanuni na Miongozo kama ifuatavyo;

(i) Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 2008,
(ii) Sheria ya Ndoa Na. 5 ya mwaka 1971,
(iii) Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009,
(iv) Sheria ya kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu Na.6ya Mwaka 2008.

3.1.1 Huduma kwa Familia

Kwa mujibu wa sheria hizi Maafisa Ustawi wa Jamii wanayo majukumu ya kuimarisha ustawi na ulinzi wa familia kwa kufanya yafuatayo:

(a) Usuluhishi wa ndoa zenye mifarakano

(i) Kufanya unasihi kwa wanandoa walio kwenye migogoro na mifarakano ili kupata suluhu ya matatizo

yanayowakabili na kuwawezesha kuishi kwa amani na upendo,

(ii) Kusimamia utekelezaji wa makubaliano yaliyofikiwa na wanandoa katika usuluhishi ili kuimarisha mahusiano baina yao na watoto wao,

(iii) Kutoa elimu kwa wanandoa/familia kabla/baada ya ndoa kwa lengo la kuwapatia stadi/kuboresha mahusiano kupitia stadi za mawasiliano; utatuzi wa matatizo; na stadi za malezi,

(iv) Kutoa rufaa kwa mashauri ya ndoa katika mahakama pale ambapo usuluhishi umeshindikana,

(v) Kujenga uwezo wa unasihi, usuluhishi na upatanishi kwa wajumbe wa mabaraza ya usuluhishi ya kata na yale ya madhehebu ya dini.

(b) Kusimamia Huduma Kwa familia zenye dhiki

Familia za watu wenye dhiki ni zile ambazo hazina uwezo wa kumudu na kukidhi mahitaji yao ya msingi kama vile chakula, mavazi na makazi kutokana na dharura zilizojitokeza au hali halisi ya maisha yao. Familia hizi ni pamoja na zile zinazoongozwa na watoto wenyewe, wazee wasiojiweza, wajane na wenye magonjwa sugu ya muda mrefu, watoto waliozaliwa wameungana na akina mama wanaopata ulemavu wakati wa kujifungua. Aidha huduma hizi hutolewa pia kwa akina mama wanaojifungua watoto zaidi ya wawili kwa mara moja. Pamoja na huduma hizo misaada mingine inayotolewa ni ile ya dharura kwa familia zenye dhiki, mahitaji ya elimu na misamaha ya huduma mbalimbali za kijamii. Shughuli wanazofanya Maafisa Ustawi wa Jamii ni pamoja na;

(i) Kupokea na kufanya uchambuzi wa maombi kutoka kwenye familia zenye dhiki pamoja na kufanya uchunguzi wa kijamii kuhusu maombi hayo,

(ii) Kutoa unasihi na ushauri wa kitaalam kwa waombaji kulingana na mahitaji au matatiza waliyonayo,

(iii) Kuzijengea uwezo familia zenye dhiki kwa kuzipatia misaada ya dharura/ midogo midogo au kuwaelekeza kwenye Taasisi nyingine ambazo zinatoa huduma/misaada wanayoomba,

(iv) Kusimamia na kufuatilia misaada iliyotolewa kwa familia zenye dhiki,
(v) Kuwezesha upatikanaji Msaada wa Rais kwa akina mama waliojifungua watoto zaidi ya wawili kwa mara moja.

3.1.2 Huduma za ustawi kwa Watoto

Kwa mujibu wa sheria Maafisa Ustawi wa Jamii wanayo majukumu ya kuimarisha ustawi na ulinzi kwa watoto kwa kufanya yafuatayo:

(a) Kusimamia Matunzo kwa watoto walio kwenye ndoa zenye migogoro;

Maafisa Ustawi wa Jamii wanasimamia matunzo kwa watoto ambao wazazi wao wako kwenye ndoa zenye migogoro ili kuwawezesha kupata haki na mahitaji yao ya msingi. Katika kusimamia jukumu hili kazi wanazofanya ni pamoja na;

(i) Kufanya uchunguzi wa kijamii ili kupata taarifa sahihi kuhusu tatizo.
(ii) Kufanya unasihi kwa wanandoa na familia ili wafikie makubaliano ya namna ya kuwatunza watoto na kusimamia utekelezaji wa makubaliano hayo.
(iii) Kuelekeza mashauri mahakamani kwa uamuzi wa kisheria endapo makubaliano ya hiari hayakufikiwa

(b) Kusimamia huduma ya matunzo kwa watoto waliozaliwa nje ya ndoa;

Huduma hii hutolewa ili watoto wanozaliwa nje ya ndoa waweze kupata haki na huduma wanazostahili. Kazi zinazofanyika ni pamoja na;

(i) Kupokea malalamiko yanayohusu matunzo kwa watoto waliozaliwa nje ya ndoa,
(ii) Kufanya uchunguzi wa kijamii kuhusu malalamiko kutoka kwa akina mama wajawazito au wenye watoto waliozaliwa nje ya ndoa na ambao baba zao hawawajibiki kuwatunza,

(iii) Kufanya unasihi kwa wahusika ili kufikia makubaliano ya hiari kuhusu matunzo na malezi ya watoto husika na kusimamia makubaliano yaliyofikiwa,
(iv) Kufanya upatanishi ili kuondoa mvutano/migogoro baina ya wazazi na kuepusha athari za kisaikolojia kwa watoto,
(v) Kuelekeza mashauri mahakamani endapo makubaliano ya hiari hayakufikiwa.

(c) Kusimamia Huduma ya Makao ya Watoto;

Huduma ya malezi, matunzo na ulinzi katika Makao hutolewa kwa watoto ambao wamekosa wazazi/ndugu na jamaa wa kuwalea kutokana na sababu mbalimbali. Huduma hii hutolewa kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto Na. 21 ya 2009 Serikali, mtu binafsi, mashirika ya hiari, mashirika ya dini, mashirika yasiyo ya kiserikali yanaweza kuanzisha na kuendesha makao ya watoto. Katika kusimamia huduma hii Maafisa Ustawi wa Jamii wanatekeleza majukumu yafuatayo;

(i) Kufanya ukaguzi wa eneo linalokusudiwa kwa shughuli hiyo,
(ii) Kufanya uchunguzi wa kijamii kwa mwombaji anayekusudia kuanzisha makao na kutoa mapendekezo kwa Kamishna wa Ustawi wa Jamii kwa ajili ya leseni ya umiliki na uendeshaji kwa muombaji aliyekidhi masharti na vigezo vya kutoa huduma,
(iii) Kusimamia na kuratibu huduma zinazotolewa kwa watoto makaoni,
(iv) Kupeleka watoto katika makao ya watoto baada ya kujiridhisha kuwa wanakidhi vigezo vya kuwekwa kwenye makao kwa mujibu wa Sheria,
(v) Kutoa idhini kwa mtoto anayetunzwa katika makao kuchukuliwa na mlezi/walezi wa kuaminika,
(vi) Kufanya uchunguzi na kutoa mapendekezo kwa Kamishna wa Ustawi wa Jamii kuwaweka watoto katika malezi ya kambo/kuasili,

(vii) Kupokea na kuchambua taarifa mbalimbali za utekelezaji na mapato na matumizi kutoka kwenye uongozi wa makao,
(viii) Kufanya ukaguzi katika makao na kutoa ushauri wa kitaalamu kila inapohitajika,
(ix) Kufanya ufuatiliaji nyumbani kwa walezi, ndugu na wazazi ili kuwaandaa kupokea mtoto/watoto wanaolelewa kwenye makao,
(x) Kuwatengamanisha watoto wanaolelewa makaoni ili waweze kujumuika na kujitegemea kwenye jamii,
(xi) Kutoa mafunzo ya malezi na ulinzi wa watoto kwa walezi wa watoto yatima na walio katika mazingira hatarishi,
(xii) Kuelimisha jamii kuhusu athari za malezi ya watoto katika makao,
(xiii) Kuhamasisha Jamii kuhusu taratibu za uanzishaji na uendeshaji wa makao ya kulea watoto.

(d) Kusimamia Huduma ya Malezi ya Kambo na Kuasili;
Huduma hii hutolewa kwa watoto ambao wamekosa malezi, matunzo na ulinzi toka kwa wazazi/walezi na ndugu kutokana na sababu mbalimbali kama vile kifo, umasikini uliokithiri na kutelekezwa. Maafisa Ustawi wa Jamii wana jukumu la kufanya kazi zifuatazo;
(i) Kufanya uchunguzi wa kijamii kwa watu wanaoomba watoto kwa ajili ya malezi ya kambo,
(ii) Kufanya uchunguzi wa kijamii kwa watoto wanaostahili kuwekwa chini ya malezi ya kambo,
(iii) Kupitia ofisi ya Kamishna Ustawi wa Jamii kufanya mawasiliano na Shirika la kimataifa la huduma za kijamii (International Social Services) kwa lengo la kupata maoni na mapendekezo kutoka Nchi za nje kuhusu waombaji ambao sio raia wa Tanzania,
(iv) Kutoa mapendekezo kwa Kamishna wa Ustawi wa Jamii ili atoe kibali cha malezi ya kambo kwa waombaji waliokidhi vigezo kwa mujibu wa Sheria.
(v) Kufanya ufuatiliaji wa malezi, makuzi na maendeleo ya watoto walio katika malezi ya kambo,

(vi) Kutoa ushauri kwa walezi wa kambo kuchukua hatua za kuasili watoto baada ya kutimiza kipindi cha miezi sita,
(vii) Kuandaa na kuwasilisha taarifa ya kijamii katika Mahakama husika kuhusu maombi ya kuasili mtoto.
(viii) Kuelimisha jamii kuhusu huduma na taratibu za malezi ya kambo na kuasili.

(e) Kusimamia Huduma ya Malezi, Makuzi Na Maendeleo Ya Awali Ya Watoto Wadogo Na Wachanga.

Huduma hii inalenga kutoa mahitaji ya msingi na uchangamshi wa awali kwa watoto wadogo walio na umri chini ya miaka mitano.

Huduma hii hutolewa kupitia programu ya malezi, makuzi changamshi ya awali ndani ya kaya na katika vituo vya kulelea watoto wadogo mchana ili kuwawezesha watoto kukua vema kimwili, kiakili, kijamii na kihisia. Huduma zinazotolewa zinajumuisha Afya, Lishe, Ulinzi na Usalama, Michezo na Burudani.Upendo, kuelekezwa maadili mema na kuandaliwa kuingia shule ya msingi. Katika kutoa huduma hizi Maafisa Ustawi wa Jamii wanatekeleza majukumu yafuatayo;

(i) Kuhamasisha jamii na taasisi mbalimbali kuhusu umuhimu wa utoaji wa huduma za malezi, makuzi na maendeleo changamshi ya awali ya watoto.
(ii) Kuandaa na kutekeleza programu za malezi changamshi ya awali kwa watoto.
(iii) Kuhamasisha Jamii kuhusu taratibu za uanzishaji na usajili wa vituo vya kulelea watoto wadogo mchana,
(iv) Kuhamasisha na kutoa ushauri wa kitaalamu wa namna ya kuanzisha na kuendesha vituo vya kijamii vya malezi wa watoto,
(v) Kufanya ukaguzi na ufuatiliaji wa huduma zinazotolewa kwa watoto wadogo na wachanga katika vituo vya kulelea watoto mchana,
(vi) Kufanya uchunguzi kwa waombaji wanaolenga kuanzisha vituo vya kulelea watoto wadogo na wachanga mchana na kutoa mapendekezo kwa

Kamishna wa ustawi wa jamii kuhusu usajili wa vituo hivyo,

(vii) Kuratibu na kusimamia uendeshaji wa vyuo vya mafunzo ya Malezi, Makuzi na Maendeleo Changamshi ya Watoto Wadogo Na Wachanga.

(f) Kusimamia Huduma ya malezi, matunzo na ulinzi shirikishi Jamii kwa watoto yatima na walio katika mazingira hatarishi

Huduma hizi hutolewa kwa watoto walio katika mazingira hatarishi, ambao wanakosa haki zao za msingi au wako katika hatari ya kukosa haki hizo. Serikali imekuwa ikitekeleza Mpango Jumuishi wa Kushughulikia Mashauri ya Watoto walio katika Mazingira Hatarishi na Familia zao tangu mwaka 2017. Huduma hizi hutolewa na Idara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali zikiwemo halmashauri, mashirika yasiyo ya kiserikali na jamii ambapo watoto hao hutambuliwa na jamii na kupata mahitaji ya msingi pale walipo. Uzoefu umeonyesha kuwa malezi kwenye familia na jamii ni bora ukilinganisha na malezi kwenye makao ya watoto ambako mara nyingi watoto huathirika kisaikologia na kijamii, pia hujenga tabia tegemezi miongoni mwao. Hivyo inasisitizwa kuwa kadri itakavyowezekana watoto watunzwe na kulelewa katika jamii zao na uamuzi wa kumpeleka mtoto makaoni iwe ni hatua ya mwisho kabisa. Kazi zinazofanywa na Maafisa Ustawi wa Jamii ni pamoja na;

(i) Kuwezesha Halmashauri ili ziweze kushirikiana na jamii kufanya utambuzi wa watoto waishio katika mazingira hatarishi na kubaini mahitaji yao, walezi wao na uwezo walionao, hatimaye kupanga mipango ya kuwahudumia,

(ii) Kujenga uwezo wa wazazi/walezi ili waweze kuwapatia watoto wao malezi bora na msaada wa kisaikolojia na kijamii,

(iii) Kushirikiana na wadau mbalimbali ili kuimarisha mifumo ya kinga ya jamii na kuziwezesha familia maskini hususan zinazolea watoto walio katika

mazingira hatarishi na hatimaye kuboresha vipato vyao ili kukidhi mahitaji ya watoto wao,

(iv) Kuziwezesha familia na jamii kuandaa mipango shirikishi jamii ya kuwahudumia watoto waishio katika mazingira hatarishi kwa kutumia rasilimali walizonazo,

(v) Kutoa mafunzo kwa walezi na watoa huduma kuhusu stadi za malezi na matunzo kwa watoto hao,

(vi) Kushirikiana na wadau mbalimbali katika kupanga mipango ya kutoa huduma na upatikanaji wa rasilimali kwa ajili ya kuwahudumia watoto hao,

(vii) Kufanya utambuzi na kutoa elimu kwa watu wa kuaminika ili kusaidia malezi na matunzo kwa watoto wenye uhitaji,

(viii) Kufanya ufuatiliaji wa malezi ya watoto wanaolelewa na watu wa kuaminika.

(g) Huduma ya Ulinzi na Usalama kwa watoto dhidi ya vitendo vya unyanyasaji, ukatili, utelekezaji na unyonyaji

Huduma hizi hutolewa kwa kuzingatia Sheria, kanuni na miongozo mbali mbali ikiwemo Mkakati wa Taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto (2017-2021). Huduma hizi hutolewa kwa watoto wahanga wa ukatili na wale walio katika hatari ya kufanyiwa vitendo vya ukatili. Katika eneo hili Maafisa Ustawi wa Jamii wana majukumu yafuatayo;

(i) Kupokea rufaa za mashauri ya unyanyasaji na ukatili kwa watoto,

(ii) Kufanya uchunguzi wa kijamii juu ya mahitaji ya mtoto na vihatarishi vinavyomzunguka,

(iii) Kuchukua hatua stahiki kwa mujibu wa Sheria ili kulinda haki na ustawi wa watoto wenye uhitaji,

(iv) Kuratibu na kusimamia uanzishaji wa kamati za ulinzi na usalama wa mtoto katika ngazi za Halmashauri, Kata na Vijiji/mitaa,

(v) Kujenga uwezo wa wazazi/walezi ili waweze kuwapa watoto malezi bora,

(vi) Kutoa msaada wa Kisaikolojia na Kijamii kwa wahanga wa ukatili na unyanyasaji wakiwemo wahanga wa Usafirishaji Haramu wa Binadamu,
(vii) Kuwapatia hifadhi ya muda wahanga wa vitendo vya ukatili na unyanyasaji wa watoto na wahanga wa usafirishaji haramu,
(viii) Kutoa unasihi na kuwaunganisha na huduma zingine kama vile msaada wa kisheria na ujasiriamali kwa wahanga wa ukatili na unyanyasaji.

3.2 HUDUMA ZA MAREKEBISHO YA TABIA NA HAKI ZA MTOTO KISHERIA

Maafisa Ustawi wa Jamii wanasimamia huduma za Marekebisho ya Tabia na Haki za Watoto Walio katika Mkinzano na Sheria na wale walio katika hatari ya kukinzana na Sheria. Huduma hizi hutolewa kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali kama ifuatavyo:

(i) Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009
(ii) Sheria ya Kanuni za adhabu (Sura ya 16) iliyorekebishwa 2002
(iii) Sheria ya Parole Na. 5 ya Mwaka 2002
(iv) Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai iliyofanyiwa Marekebisho 2002

3.2.1 Kusimamia Haki za Mtoto Kisheria

Kwa kuzingatia sheria hizi, Maafisa Ustawi wa Jamii wana majukumu ya kusimamia utekelezaji wa huduma zifuatazo:

(i) Kuhakikisha watoto wanaoshitakiwa kwa makosa ya jinai wanapelekwa katika mahakama za watoto Kuhakikisha watoto wanapelekwa katika mahabusi za watoto badala ya mahabusu za wakubwa, pale ambapo wamekosa dhamana au kosa lake halistahili dhamana,
(ii) Iwapo watoto wanapatikana na hatia kwa kosa la jinai na iwapo umri wao ni chini ya miaka 16, Afisa Ustawi wa Jamii atawasilisha taarifa mahakamani. Taarifa hii itamwezesha Hakimu kupata picha kamili kuhusu maisha na mazingira ya mshitakiwa kabla ya kutoa hukumu.

Taarifa hii pia itamsaidia Hakimu kutoa hukumu ya kumpeleka mtoto chini ya usimamizi na uangalizi wa Afisa Ustawi wa Jamii kwa muda usiopungua miezi 12 na usiozidi miezi 36, au atahukumiwa kwenda katika Shule ya Maadilisho kwa muda kati ya miezi 12 na 36 badala ya kuhukumiwa kwenda kutumikia kifungo chake katika jela za watu wazima. Aidha Afisa Ustawi wa Jamii kutokana na mazingira ya mtoto anaweza kupendekeza kutolewa kwa rufaa ili mtoto achepushwe na kupelekwa kwenye mpango wa kijamii wa marekebisho ya tabia,

(iii) Kusimamia huduma katika Mahabusu za watoto ikiwemo kuwahifadhi na kuwatunza katika mahabusu ili kutoa ulinzi na usalama,

(iv) Kushirikiana na Jamii katika kutoa huduma muhimu za malezi na maadili mema kwa kuzingatia haki za watoto kwa lengo la kurekebisha tabia,

(v) Kuwaunganisha watoto na familia /jamii zao.

3.2.2 Kusimamia Huduma za Marekebisho ya Mtoto

Maafisa Ustawi wa Jamii wana jukumu la kusimamia huduma za Marekebisho ya Tabia kwa watoto walio katika mkinzano na Sheria na wale walio katika hatari ya kukinzana na Sheria. Katika kutekeleza jukumu hili, Maafisa Ustawi wa Jamii wanatoa huduma zifuatazo:

(i) Kuwezesha watoto kwenda Shule ya Maadilisho kwa amri ya Mahakama,

(ii) Kuwaunganisha waadiliwa na huduma muhimu kama vile elimu ya msingi, stadi za maisha na ushauri nasaha,

(iii) Kufanya utengamao kwa waadiliwa na kuwaunganisha familia/ jamii,

(iv) Kufanya unasihi na kutoa msaada wa kisaikolojia kwa waadiliwa ili kusaidia kurekebisha tabia zao,

(v) Kutoa rufaa kwenda kwenye mpango wa kijamii marekebisho ya tabia.

3.2.3 Kusimamia huduma kwa watoto watukutu

Maafisa Ustawi wa Jamii wana jukumu la kusimamia huduma za marekebisho kwa watoto watukutu. Katika kutekeleza jukumu hili, wanatoa huduma zifuatazo:

(i) Kufanya uchunguzi wa tabia na mwenendo wa watoto watukutu ili kufahamu sababu zinazosababisha mwenendo mbaya kwa watoto hao,

(ii) Kufanya unasihi na kutoa msaada wa kisaikolojia kwa watoto na wazazi wao ili kuboresha malezi kwa watoto,

(iii) Kufanya marekebisho ya tabia za watoto kwa kuwahusisha katika michezo, elimu ya ufundi, unasihi, stadi za maisha na shughuli mbalimbali kutegemea na mazingira walipo kwa lengo la kutatua tatizo la utukutu.

3.2.4 Kusimamia huduma za ustawi katika Mahakama za Watoto

Maafisa Ustawi wa Jamii wana jukumu la kusimamia huduma za ustawi kwa kufanya yafuatayo:

(i) Kufanya uchunguzi na kuandaa taarifa ya kijamii,

(ii) Kuwasilisha taarifa hiyo Mahakamani ili kumsaidia Hakimu kutoa maamuzi kwa maslahi ya mtoto,

(iii) Kuandaa na kutekeleza mpango wa marekebisho ya tabia ya mtoto.

(iv) Kusimamia na kufuatilia mwenendo na tabia za mtoto,

(v) Kuwaunganisha watoto na wazazi/walezi.

3.2.5 Kusimamia Huduma kwa watoto wanaoishi na kufanya kazi Mitaani

Watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani ni moja ya makundi ya watoto walio katika mazingira hatarishi. Kutokana na mazingira wanayoishi yanawaweka katika hatari ya kuingia katika mkinzano na sheria kutokana na kutokuwa na uangalizi na uhakika wa kupata mahitaji muhimu kama vile chakula, mavazi na malazi. Maafisa Ustawi wa Jamii wana jukumu la kusimamia huduma kwa watoto hawa na kuhakikisha ulinzi na ustawi wao unaimarishwa. Huduma zinazotolewa ni pamoja na:

(i) Kusimamia vituo vinavyotoa huduma kwa watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani,

(ii) Kubuni mipango ya kusaidia kuzuia ongezeko la watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani,
(iii) Kuratibu shughuli na huduma zinazotolewa na taasisi za hiari kwa watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani,
(iv) Kufanya uchunguzi wa vituo vinavyolenga kutoa huduma kwa watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani,
(v) Kukagua na kutoa ushauri wa kitaalam kwa taasisi na watumishi wanaoshughulika na utoaji wa huduma kwa watoto wanaoishi mitaani,
(vi) Kufanya mapitio ya maombi ya usajili wa vituo na kuwasilisha kwa msajili,
(vii) Kufanya uchunguzi wa kijamii na kuwaunganisha/kuwatengamanisha watoto hao na wazazi/walezi wao.

3.3 HUDUMA KWA WAZEE NA WATU WENYE ULEMAVU

Huduma kwa Wazee Wasiojiweza na Watu wenye Ulemavu hutolewa kwa mujibu wa Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo mbali mbali ya kitaifa na kimataifa inayolenga katika kuhakikisha huduma muhimu za malezi, matunzo na ulinzi zinawafikia. Aidha, Serikali imeridhia mikataba mbalimbali ya kimataifa inayolenga katika utoaji wa haki na ustawi kwa wazee na Watu Wenye Ulemavu na hivyo kulazimika kuweka mazingira bora na wezeshi ya upatikanaji wa huduma hizo kwa makundi hayo. Huduma hizi hutolewa kwa kuzingatia Sera na Sheria zifuatazo:

(i) Sera ya Taifa ya Wazee (2003)
(ii) Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu (2004).
(ii) Sheria ya Watu Wenye Ulemavu (Na. 9, ya 2010)

Maafisa Ustawi wa Jamii wana majukumu yafuatayo katika eneo hili:

(i) Kuwatambua na kuwaunganisha wazee na watu wenye ulemavu na huduma za msingi kama vile matibabu, misaada ya kiuchumi ili kuondoa umaskini,

(ii) Kuratibu upatikanaji wa nyenzo za kujimudu kwa watu wenye ulemavu, ikiwa ni pamoja na vifaa vya kutembelea, baiskeli za magurudumu matatu, viatu maalum, shime sikio, miwani, fimbo nyeupe, kofia, miguu na mikono ya bandia,

(iii) Kuandaa Mafunzo ya Stadi za kazi kwa wazee wasiojiweza na Watu Wenye Ulemavu,

(iv) Kubuni na kutekeleza mipango ya Utengamao kwa wazee wasio jiweza na Watu Wenye Ulemavu,

(v) Kutoa Huduma za Marekebisho kwa Watu Wenye Ulemavu,

(vi) Kusimamia Matunzo kwa wazee na Watu Wenye Ulemavu/Wasiojiweza,

(vii) Kutoa ushauri katika huduma za Utengamao kwa Wazee walio katika Makazi ya Wasiojiweza,

(viii) Kutoa ushauri juu ya Huduma za ustawi na haki kwa Wazee kama vile uanzishaji na usimamizi wa mabaraza ya wazee,

(ix) Kuratibu uandaaji wa taarifa za ustawi wa jamii kuhusu wazee na watu wenye ulemavu,

(x) Kuratibu uchambuzi wa maombi ya misaada kutoka kwa wazee na watu wenye ulemavu,

(xi) Kutambua na kufanya tathmini kwa wazee na watu wenye ulemavu wenye magonjwa sugu ili kuwaunganisha na huduma stahiki,

(xii) Kutambua na kutoa mapendekezo ya msamaha wa matibabu na huduma nyingine za ustawi wa jamii kwa wazee wasiojiweza kwenye zahanati, vituo vya afya na Hospitali,

(xiii) Kuratibu utoaji wa elimu katika jamii juu ya masuala mbalimbali ya wazee na watu wenye ulemavu,

(xiv) Kujenga mtandao na ushirikishwaji wa wadau mbalimbali katika masuala yanayohusu wazee na watu wenye ulemavu,

(xv) Kutunza regista na kuhuisha kumbukumbuku za wahudumiwa,

(xvi) Kutoa huduma ya kisaikolojia na kijamii kwa wahudumiwa.

4.0 MAJUKUMU MENGINE MTAMBUKA

(i) Kuandaa mpango kazi wa mwaka kulingana na bajeti ya shughuli za Ustawi wa Jamii,

(ii) Kutoa ushauri na mapendekezo kwa mamlaka husika katika masuala ya Ustawi Wa Jamii,

(iii) Kutoa elimu katika jamii juu ya masuala mbalimbali ya ustawi wa jamii.

(iv) Kujenga mtandao na ushirikishwaji wa wadau mbalimbali katika masuala yanayohusu Ustawi wa Jamii,

(v) Kuandaa na kutekeleza mpango wa huduma kwa wahudumiwa,

(vi) Kutunza rejista na kuhuisha kumbukumbu za huduma za Ustawi wa Jamii.

(vii) Kutoa msaada wa kitaalamu na kusimamia wanafunzi wa ustawi wa jamii wakati wa mafunzo kwa vitendo,

(viii) Kufanya tafiti za kijamii kwa ajili ya kuboresha utoaji huduma za ustawi wa jamii,

(ix) Kupokea, kukusanya na kuchambua takwimu, kufanya ukaguzi/tathmini, kutunza kumbukumbu na kuandaa taarifa za wahudumiwa wa ustawi wa jamii na mazingira yao,

(x) Kuratibu uandaaji wa mpango kazi wa mwaka kulingana na bajeti Kuratibu uandaaji wa taarifa ya kazi za kila siku na kutoa taarifa za Maendeleo za Robo mwaka, Nusu mwaka na Mwaka,

(xi) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya shughuli zote za ustawi wa jamii.

5.0 MAADILI YA AFISA USTAWI WA JAMII

Miongozo ya Shirikisho la Kimataifa la Wataalamu wa Ustawi wa Jamii (International Federation of Social Workers) imeainisha maadili kwa maafisa ustawi wa jamii ambayo yanajengwa katika msingi wa Maadili ya Utumishi wa Umma. Maadili hayo ni pamoja na:

(i) Kuheshimu na kumkubali kila mteja anayemhudumia,

(ii) Kutunza siri za mteja na siri za Ofisi,

(iii) Kutoa huduma kwa weledi na kuzingatia mipaka ya taaluma na mamlaka alizopewa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni,

(iv) Kutoa huduma bila upendeleo,

(v) Kuheshimu na kuendeleza haki ya mteja kufanya maamuzi na kumsaidia kutafsiri malengo yake,

(vi) Kujenga mahusiano mema ya kikazi na mteja na kutumia lugha fasaha na rahisi kumuelewesha mteja kuhusu malengo ya huduma na athari zake,

(vii) Kutoa huduma kwa misingi ya haki na usawa kwa kujali utu wa kila mteja,

(viii) Kuheshimu mawazo ya mteja,

(ix) Kuheshimu mila na tamaduni na kutambua athari zake katika tabia za watu na jamii,

(x) Kuepusha migongano ya kimaslahi ambayo itaingiliana na maamuzi ya kitaaluma,

(xi) Kutojihusisha na mahusiano/shughuli za kimapenzi na mteja au ndugu/watu waliokuwa na mahusiano ya karibu na mteja wakati wa shauri lake,

(xii) Kutotoa wala kupokea rushwa.

6.0 HATUA MUHIMU ZA KUFUATA WAKATI WA UTENDAJI KAZI

Afisa Ustawi wa Jamii anatakiwa kuwahudumia wateja wake kwa kufuata miongozo, kanuni na Sheria zinazoongoza utoaji wa huduma za ustawi wa jamii nchini. Baadhi ya hatua muhimu zinazopaswa kufuatwa ni pamoja na;

(a) Kupokea shauri/kusajili/kusaili mashauri ya wateja,
(b) Kufanya uchunguzi wa awali,
(c) Kufanya uchunguzi wa kina,
(d) Kuandaa Mpango wa huduma,
(e) Kutekeleza na kufuatilia Mpango wa huduma,
(f) Kutoa rufaa, na kufunga/kuhamisha shauri.

7.0 HITIMISHO

Mwongozo huu utawezesha Maafisa Ustawi wa Jamii kubaini mipaka yao ya kiutendaji, kuongezeka kwa morali ya kufanya kazi, na kupata uelewa mpana kuhusu utoaji wa huduma za ustawi wa jamii kulingana na ngazi husika. Aidha Mwongozo huu utawezesha Viongozi na Watendaji wengine katika Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kufahamu kwa kina majukumu ya Maafisa Ustawi wa Jamii katika ngazi zao.

Mwongozo huu pia utawezesha kuondoa changamoto katika utelkelezaji wa majukumuwakati wa kutoa huduma za ustawi wa jamii hapa nchini na kuwezesha kuwa na jamii iliyostawi na kuyawezesha makundi maalum kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya nchi.

KIAMBATISHO; Mfumo wa Utoaji Huduma za Ustawi wa Jamii katika Halmashauri